





Tarik na familia
yake waliishi mbali
na mji mkuu.



Tarik alikuwa na
mbwa aliyeitwa
Buchi.

Walikuwa marafiki
wakubwa.



Siku moja, Tarik na
rafiki yake Bedilu
waliwapeleka
mifugo malishoni.



Bedilu alipenda
wacheze, lakini
Tarik alitaka kusoma.




Mwishowe, Bedilu na
Tarik waliamua kucheza.



Walipokuwa wakicheza,
kondoo walitoweka.

Waliwatafuta kila mahali.



Mbwa mwitu aliuua
kondoo wa Tarik.

Tarik aliogopa kuadhibiwa
na baba yake.



Tarik aliamua kulala
juu ya mti.

Buchi alilala karibu na
mti huo.



Usiku, fisi walipiga
kelele Tarik akaogopa.



Tarik alianguka kutoka
mtini.

Alisikia kelele karibu naye.



Wakati huo, radi
ilimlika anga.

Tarik alimwona
Buchi akiwa anamlinda!



Tarik na Buchi waliketi
juu ya mti hadi asubuhi.